



# Mzozo wa Nyumbani na Kifamilia

## Nchini Australia, Mzozo wa Nyumbani na kifamilia haukubaliki.

Mzozo wa Nyumbani na kifamilia ni uhalifu wa kinyume cha sheria.

Mtu anayetenda uhalifu huu anaweza kwenda jela, awe mwanamume au mwanamke.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, piga simu kwa polisi, nambari ya simu **000**.

Polisi nchini Australia ni salama na wanaweza kuaminika.

Kwa ushauri na maelezo ya bila malipo na ya siri, piga simu kwa 1800RESPECT, nambari ya simu **1800 737 732**.

Ikiwa unahitaji mkalimani bila malipo piga simu kwa **131 450**.

## Australian Government (Serikali ya Australia) haivumilii Mzozo wa Nyumbani na familia chini ya hali yoyote ile.

Mzozo wa nyumbani na familia ni pamoja na tabia au vitisho ambavyo vina lengo la kudhibiti mpenzi na kusababisha hofu au kutishia usalama wao. Mzozo wa Kinyumbani na familia unajumuisha:

- kupiga;
- ugomvi.
- kunyima fedha muhimu kwa mpenzi au familia;
- kumtenga mpenzi kutoka kwa marafiki na familia;
- matusi au kukosoa mpenzi mara kwa mara;
- kumlazimisha mpenzi kufanya mapenzi; na
- kutishia watoto au mifugo.

## Wanawake wana haki sawa na wanaume.

Sheria za Australia zinachukulia wanawake na wanaume kuwa sawa.

Kila mtu ana haki ya kuwa katika mahusiano mazuri na salama na familia, marafiki na wapendwa wao. Unyanyasaji si sawa hata kidogo. Hakuna yeyote anapaswa kukubali kutendewa vibaya au kuumizwa.

## Kuna huduma za kijamii nchini Australia ambazo zinaweza kukusaidia.

**1800RESPECT** ni huduma ya ushauri wa mzozo wa kijinsia, uhasama wa kifamilia na kinyumbani kutoka kwa taifa la Australia (Australia's national sexual assault, family and domestic violence counselling service). Hutoa maelezo na ushauri wa mtandaoni na wa simu bila malipo na wa siri. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za msaada katika eneo lako.

Piga simu kwa **1800 737 732** au nenda kwenye **tovuti ya 1800RESPECT** kwenye **www.1800RESPECT.org.au**.

## Je unahitaji mkalimani?

Piga simu kwa **Huduma ya Ufasiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS))**, nambari ya simu **131 450**. Mkalimani kutoka TIS anaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma zingine, hata hivyo TIS haitoi huduma ya ushauri. Simu zote hazilipishwi na ni za siri.